**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE-2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari KIBAKWE**

**S.L.P. 243**

**MPWAPWA**

**Tarehe .11/04/2024**

**Namba za simu**

**Mkuu wa Shule: 0784221038**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0684128333**

**Mwalimu wa malezi : 0758039695**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE HALMASHAURI YA MPWAPWA MKOA DODOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule yetu ipo Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Mpwapwa, jimbo la Kibakwe. Mji wa Mpwapwa unafikika kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dodoma. Upo usafiri wa kila siku kutoka Dodoma ambao hufanya safari zake kuanzia saa 03:00 asubuhi na saa 09:00alasiri. Usipopata usafiri wa aina hii, unaweza kupanda mabasi yanayoelekea Gairo, Morogoro au Dar Es Salaam na kushuka kituo cha ***Mbande***, mahali ambapo ni njia panda ya kuelekea Mpwapwa na Kongwa. **Tafadhali sana usipande gari au basi linaloekea Kongwa, subiri linaloelekea Mpwapwa.**

Endapo unatokea Dar Es Salaam au Morogoro unashauriwa kutumia basi lolote kati ya mabasi yanayofanya safari zake kuja Mpwapwa moja kwa moja; usafiri huu upo kila

siku,ukikosa basi la moja kwa moja tumia basi lolote linaloelekea Dodoma na uteremkie Mbande na kupata usafiri wowote unaolekea Mpwapwa. **Unatahadharishwa tena kutotumia magari yanayoishia Kongwa.**

Kwa wale watakaotumia usafiri wa treni, tunashauri kuteremkia Dodoma mjini ambapo ni rahisi kupata usafiri wa kuelekea Mpwapwa mjini moja kwa moja. Mabasi yanayokuja Mpwapwa huanzia safari zake Dodoma Mjini kwenye kituo kiitwacho ***SOKO LA NDUGAI.***

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 1 JULAI 2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30 JUNI 2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30 JUNI 2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

**WASICHANA**

- **i.** Shati/blauzi nyeupe mbili za tetroni ya mikono mifupi, sketi mbili za heshima za rangi ya dark blue zenye malinda **14 hadi 16** na urefu hadi kwenye kisigiono **NA SIYO KUSHONA V BOX**
- ii. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na rangi)
- **iii.** Sweta la rangi ya dark blue na soksi nyeupe jozi mbili**.**
- **iv. Muislamu akiona inafaaa ” hijab’’ inaruhusiwa ambayo atavalia na sketi ndefu inayofika kwenye kisigino yenye marinda 14-16 . Jacket haliruhusiwi kabisa.**
- **v.** Nguo ya kushindia (shamba dress) ni sketi **RANGI YA JANI LA MGOMBA YENYE MARINDA 14-16 NA UREFU HADI KWENYE KISIGIONO**.
- **i.** Tisheti mbili (T-shirt) yenye rangi nyekundu yenye nembo ya shule ambayo ataikuta hapa shuleni na inapatikana kwa gharama ya shilingi elfu kumi na tano kwa moja.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

- i. Madaftari 9 (counter book Quire 4 )
- ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
- iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika orodha imeambatanishwa
- iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
- v. Scientific Calculator; kwa wanafunzi wa CBG NA HGK
- vi. Godoro Size ya godoro ni 6 x 2.5 x 6”
- vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue na pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe*;*
- viii. Nguo za ndani za kutosha;
- ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
- x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
- xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje na dawa ya chooni aina ya ”careline” lita 5
- xii. Tranka kwa ajili ya kuwekewa vitu vyake.

xiii. Results slip ya Kidato cha Nne

**Ili kurahisisha utamaji wa fedha kwa mwanafunzi, mara mtoto atakapofika hapa atafunguliwa akauti ya NMB au CRDB na mzazi utatuma fedha kupitia akaunti hizo kwa ajili ya matumizi ya mtoto.**

Mwanafunzi afike na barua hii pamoja na fomu ya kukubali kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe na cheti cha Daktari wa hospitali ya Serikali kuthibitisha afya yake (**tafadhali usifiche kama mwanao ana tatizo la kiafya)** .Vitu hivi pamoja na vingine alivyoagizwa atavionesha au kuvikabidhi wakati wa kuripoti Shuleni.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo yote yalipwe kupitia Benki ya NMB tawi lolote au Wakala yeyote nchini kwa kupitia akaunti namba **50401100039** yenye jina la **'(KIBAKWE SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION).** Stakabadhi zote za malipo (bank pay-in-slip) ziletwe Shuleni zikiwa na jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake nyuma.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE**

**SAJIGWA G. NIKUPALA**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0784221038**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0684128333**
- **Mwandamizi Taaluma: 0694385490**
- **Mwandamizi Malezi : 0758039695**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBAKWE

A. Mimi mwanafunzi…………………………………………...(majina matatu) wa SLP;……………………………................................................... nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Kibakwe pamoja na Sheria na Kanuni zake. Nimeelewa vema nami naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati wote nitakapokuwa shuleni na mahali pengine popote. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote na nisome kwa bidii ili nipate elimu bora. Nitakuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa ajili ya maendeleo yangu,ya shule na Taifa zima kwa jumla.

**Sahihi ……………………………….** **Tarehe:……/……/ 20….**

B. Mimi…………………………………..……………....Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi:

……………………………………………………nimesoma maagizo ya kujiunga na

Shule ya Sekondari Kibakwe pamoja na sheria na kanuni za shule. Naahidi nitamsaidia \ mwanafunzi huyu kwa hali na mali ili aweze kukamilisha masomo yake ya sekondari bila kipingamizi chochote.

Na nipo tayari kufikishwa kwenye vyombo vya dola endapo nitashindwa kumtimizia kijana wangu mahitaji yake ya msingi yaliyoorodheshwa kwenye barua ya kujiunga na Kidato cha Tano. Na maandishi haya yatumikekama ushahidi dhidi yangu.Nitashirikiana na Uongozi wa Shule ili kutimiza azma hii. Kama sitapatikana tafadhali wafuatao (ndugu watatu) waitwe shuleni pakitokea tatizo au kitu kingine chochote kitakachohitaji uwepo wangu.

**Ndugu wa kwanza** …………………………………………… picha

Namba ya simu ……………………………

**Uhusiano wake na mwanafunzi(kaka,dada,shangazi,mjomba,shemeji…)**

….……………………………………………………

**Ndugu wa pili**……………………………………………

Namba ya Simu ……………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………

**Ndugu wa tatu** ……………………………………………

Namba ya Simu……………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi……………………….

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPWAPWA DISTRICT COUNCIL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**FROM HEADMASTER KIBAKWE SECONDARY SCHOOL**

**P.O.BOX 243, MPWAPWA**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**NAME OF STUDENT:……………………………….…………………….AGE…………**

**MEDICAL HISTORY**

| | YES | NO |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Peptic ulcers | | |
| Epilepsy | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidney problem | | |
| Anaemia | | |
| Neurosis | | |

**PHYSICAL EXAMINATION:**

Respiratory system -
Cardiovascular system -
Gastrointestinal system -

Urinary system -

Reproductive
system - Eye: R

**INVESTIGATION**

1. Blood -HB……………………
   -WBC………………….
   -ESR……………………
   -VDRL Test……………
2. Urine – Pregnancy………………………..
   -Sed…………………………………
   -Stool……………………………….

I have examined the above student and considered that he/she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Signature………………………………….. Designation;…..……………………….

Station;…………………………………… Date;………………………………

## VITABU WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI.

Vitabu ambavyo vinatumika hapa shuleni ni kutoka **TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TIE)**. Mzazi unashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo aliyopangiwa mtoto wako.